

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE

SHULE YA SEKONDARI BUNA

Kumb. Na.BSS/FYK/KDT I/2021

Ndg

.....

.....

YAH: MAAGIZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA
KWANZA 2021

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule hii. Nakupongeza sana kwa kuchaguliwa na nategemea utaitumia nafasi hii ipasavyo ili kujenga historia nzuri ya maisha yako. Ni mategemeo ya shule kuwa uwapo hapa utashirikiana vizuri na walimu, Watumishi wasio walimu na wanafunzi wenzako kufanya kazi za darasani na nje ya darasa. Unatakiwa kufika shuleni tarehe **11/01/2021**. ili kuanza masomo yako kikamilifu.

SARE ZA SHULE

WAVULANA

- Shati mbili nyeupe kabisa tetron zenye ukosi wa kawaida, mikono mifupi pamoja.

- Suruali ya RANGI YA KIJANI YA JESHI(kitambaa kimewekwa katika fomu hii) upana wa chini uwe wa inchi 18, iwe na rinda mbili kila upande na mifuko mitatu, mkanda wa kuvalia suruali uwe wa ngozi rangi nyeusi (chuma cha kwenye mkanda kisiwe na urembo na maandishi ya aina yoyote,pia usiwe utambi)

- Viatu vyeusi jozi mbili, visiwe buti, viwe vya kamba. Viatu visivyofungwa na kamba havikubaliki/haviruhusiwi.

- Jozi mbili za soksi nyeusi.

WASICHANA

-Chati mbili nyeupe kabisa za tetron zenye ukosi wa kawaida, kwa wanaovaa hijabu ni nusu kanzu nyeupe na kijuba cheupe urefu uwe katika kiwiko cha mikono.(kiwe cha kuchonwa) .

-Sketi mbili za rangi ya KIJANI YA JESHI zenye linda box mbele na nyuma (kitambaa kimeambatanishwa katika fomu hii)

-Soksi nyeupe jozi mbili na viatu nyeusi vya kamba.

MAHITAJI YA KITAALUMA

-Uje na daftari kubwa (Counter books) zisizopungua 12, mathematical set na kamusi ya Kiswahili –kiingereza ili kuwezesha kijifunza kiingereza,mathematical set ,peni na penseli, rula n.k

CHAKULA

Unatakiwa kuchangia chakula kwaajiliyas mlo wa mchana kama ifuatavyo,

-Mahindi yaliyokobolewa 5 kilogram

-Maharagwe mekundu 2 kilogram

-Na tsh 1000/- ya mpishi na viungo vingine kama mafuta n.k (michango hii ni kwa kila mwezi)

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

- Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978.
- Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.
- Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

- (a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule ndani na nje ya shule ni LAZIMA.
- (b) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (c) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (d) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- (e) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (f) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- (g) **MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU KIPINDI CHOTE AWAPO SHULENI.**

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI.

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga
3. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya. kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nakadhalika.
4. Uvutaji bangi na sigara
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoja/kusababisha mimba
10. Kulawiti
11. Utoro
12. Kutofanya mazoezi au mitihani ya masomo na kutega vipindi
13. Kiburi na ukaidi
14. Kugoma/kuchochea na kuongoza mgomo
15. Kukataa adhabu kwa makusudi
16. Kumiliki/kutumia simu shuleni
17. Kuchelewa kufika shuleni baada ya shule kufungwa na kutoroka kabla ya shule kufungwa

AKSANTE NA KARIBU SANA

REHEMA B. ALLY(0714-138050)

.....

MKUU WA SHULE

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL AND LOCAL GOVERNMENT
KOROGWE DISTRICT COUNCIL
BUNASECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officers in a recognized Hospital in respect of all new entrants of Buna Secondary School

Full Name.....

Age.....

1. Blood comment (red & white).....

3. Urine examination.....

4. Stool examination.....

5. Syphilis test.....

6. T.B. test.....

7. Ear test.....

8. Spleen.....

9. Abdominal

10. Eye test.....

11. Additional information or any other physical, hereditary or infectious diseases

.....
.....
.....

Treatment after examination

.....
.....
.....

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue for further education

Signature.....

Designation.....

Station.....

Official stamp.....

Date.....

N.B Fomu hii ijazwe na Mganga katika Hospitali inayotambulika na Serikali.